# I.Habari kuhusu bidhaa

# Mada ya 7

# Mwongozo wa kushughulikia mbolea

# JARIDA LA UHAKIKA

## I. Habari kuhusu bidhaa

## <u>Mada ya 7:</u> Mwongozo wa kushughulikia mbolea

**Kushughulikia mbolea**
Mbolea ina hatari ndogo sana kwa binadamu, mazingira, na maji ilio chini ya ardhi kama itashughulikiwa na kuhifadhiwa kwa njia sahihi. Kuzuia uchafuzi utokao kwa mbolea ndio njia mwafaka ya kukinga maji ardhini na mazingira.

**Vya kufanya na vya kutofanya katika kushughulikia mifuko ya mbolea**

- Nunua tu mbolea ya kutosha matumizi ya wakati huo. Usinunue kiasi kinachozidi mahitaji yako.
- Chunguza kama mifuko ina mashimo kabla ya kuipokea kutoka kwa muuzaji. Usikubali mifuko iliohariibika.
- Rekebisha mifuko ilio na mashimo mara moja. Mbolea ikimwagika, ishughulikie mara moja. Fagia pamoja mbolea hiyo. Kama haijachanganyika na vitu vingine, irudishe mfukoni. Usiuze mbolea kama imechafuliwa, itupe kwa njia ilio salama.
- Weka mbolea juu ya mbao wala sio juu ya sakafu za saruji.
- Tumia vitita tofauti kwa kuhifadhi aina tofauti za mbolea ya mifukoni. Wacha nafasi katikati ya kila aina tofauti za mbolea ya mifukoni.
- Epuka kushughulikia mbolea za mifukoni kama sio lazima ili kupunguza uwezekano wa kuharibu mifuko.
- Fuata kanuni ya mfuko wa kwanza kuhifadhiwa, ndio wa kwanza kutolewa. Weka mifuko mipya nyuma na mizee mbele ya hifadhi. Uza mifuko mizee kwanza.
- Tunza maghala ya mbolea vizuri. Yasafishe na uyakague mara kwa mara. Fundisha wafanyikazi na uangalie ilani za maonyo.
- Hakikisha mbolea zote zina vibandiko kamili vya maelezo.
- Weka rekodi nzuri ya mbolea ilio kwenye maghala
- Hakikisha wafanyikazi kwenye maghala wanatumia mavazi ya kujikinga
- Usihifadhi mbolea pamoja na petroli, mafuta na gesi.
- Usikubali watu wasio na idhini kwenye maghala ya mbolea

# MAELEZO YA ZIADA

## I. Habari kuhusu bidhaa

## Mada ya 7: Mwongozo wa kushughulikia mbolea

**Mwongozo wa kushughulikia mbolea**

1. **Mbolea zilizo kubwa/nyingi za majimaji:**
    - Hifadhi mbolea hizi katika matangi yasiolika
    - Hakikisha mabomba, unganisho za tangi na vali/vilango viko katika hali nzuri.
    - Usiweke mbolea hii katika matangi yalioko chini ya ardhi.
    - Kila tangi la mbolea hii lazima liwekwe vibandiko vya maelezo.

2. **Mbolea kubwa/Nyingi ilio kavu:**
    - Weka mbolea hii kwenye sakafu sisizopenya chini ya paa, ndani ya pipa au ndani ya jengo kamili.
    - Hakikisha aina tofauti za mbolea zinahifadhiwa zikiwa na nafasi kati yake.
    - Hakikisha mbolea hii imekingwa kutoka kwa unyevu na maji.
    - Kila aina ya mbolea hii lazima iwe na vibandiko vya maelezo.

3. **Mbolea za majimaji:**
    - Kuwa mwangalifu na mbolea za aina hii kwa sababu uwezekano wa kuvuja na kumwagika ni wa juu sana kuliko mbolea kavu.
    - Hakikisha vyombo na vifuniko havivuji
    - Vyombo visikuwe na kutu au ulikaji
    - Vyombo vyote viwe na vibandiko vya maelezo.

**Mwongozo wa kuchanganya mbolea**

- Eneo la kuchanganyia mbolea liwe karibu sana na ghala.
- Eneo la kuchanganyia liwe mbali na mito na pasipokuwa rahisi kufikia maji ya ardhini.
- **Mbolea kavu** yafaa kuchanganyishiwa kwenye sakafu kavu isioweza kupenyesha maji na ambayo ina ukubwa wa kutoshea mbolea inayochanganywa. Fagia eneo hili mara moja tu baada ya kuchanganya. Mbolea yote iliochanganywa lazima iwekwe kwenye chombo cha kuwekea shambani. Changanya tu mbolea inayotosha matumizi ya wakati huo.

- **Mbolea ya majimaji** yafaa kuchanganyishiwa kwenye sakafu kama ya saruji. Nyufa zote kwenye sakafu lazima zizibwe kabla ya kutumia sakafu hiyo. Fagia eneo hili mara moja tu baada ya kuchanganya. Mbolea yote iliochanganywa lazima iwekwe kwenye chombo cha kuwekea shambani. Changanya tu mbolea inayotosha matumizi ya wakati huo.

**Maswali ya kuzingatia unapotathmini maghala ya kuhifadhi mbolea**

- Maji ya ardhini na yalio wazi ya karibu iko salama?
- Ni mara ngapi tunakagua maghala na yaliomo ndani yake?
- Maeneo ya kuchanganyia na upakiaji ni ya kiwango kinachohitajika?
- Mavazi ya kujikinga yako?
- Je, shughuli zote zinarekodiwa kiusawa?
- Je, tumejiandaa kwa hali ya dharura?

# MWONGOZO

## I. Habari kuhusu bidhaa

## <u>Mada ya 7:</u> Mwongozo wa kushughulikia mbolea

### Vifaa vinavyohitajika:

- ☑ Ubao ulio na makaratasi
- ☑ Markers (1 nyeusi, 1 bluu, 1 kijani, 1 nyekundu)
- ☑ Kadi za rangi (1 blue card and 1 yellow card for every participant)

### Muda unaohitajika: Dakiki 30

### Maandalizi:

- ☑ Makaratasi ya kufungua kurasa yalio na kichwa *Mwongozo wa kushughulikia mbolea*
- ☑ Makaratasi ya kufungua kurasa yalio na kichwa *Fanya…* na hoja zifuatazo:
  - *Rekebisha mifuko ilio na mashimo*
  - *Panga mbolea aina tofauti katika vitita tofauti*
  - *Kanuni ya kwanza ndani – kwanza nje*
  - *Utunzaji ghala ulio bora*
  - *Weka vibandiko vya maelezo sahihi*
  - *Hifadhi rekodi zilizo bora*
  - *Tumia mavazi ya kujikinga*
- ☑ Makaratasi ya kufungua kurasa yalio na kichwa *Usifanye/Usi…* na hoja zifuatazo:
  - *Nunue kushinda mahitaji yako*
  - *Kubali mifuko iliharibika*
  - *Weke vitita kwenye sakafu ya saruji kavu*
  - *Shughulikie mbolea ya mifuko kama sio lazima*
  - *Weke mbolea pamoja na petroli, mafuta au gesi.*
  - *Kubali watu wasio na idhini kuingia ghalani.*

## Mwanzo

| | |
|---|---|
| **U**sikivu: | Waulize washiriki mahali wanapohifadhi bidhaa za vyakula na matumizi ya nyumbani. Watakuwa na majibu tofauti: kabati, jikoni, stoo ya chakula na kadhalika. |
| **K**ichwa**:** | Waambie washiriki kichwa huku ukiwaonyesha karatasi ya kufungua kurasa ilio na kichwa: Mwongozo wa kushughulikia mbolea. |
| **K**usadikika: | Elezea uzoefu wako kuhusu mwongozo wa kushughulikia mbolea. |
| **M**alengo: | Kuelezea kushughulikia kulio sahihi kwa mbolea ya mifuko. |
| **M**anufaa: | Kuelewa ushughulikiaji sahihi wa mbolea kutawasaidia wachuuzi wa bidhaa za ukulima kudhibiti bidhaa zao na kuepuka uharibifu kwa mifuko ya mbolea na upotevu wa pesa. |
| **M**welekeo : | Katika kipindi hiki, tutaangazia mwongozo wa kushughulikia mbolea ya mifuko. Hatutajadili mwongozo wa mbolea ya majimaji au ilio kwa wingi/ukubwa. |

# Wasilisho

## **U**fafanuzi, **M**aonyesho, **M**azoezi, na **M**wongozo:

1. Waambie washiriki kwamba walikwambia wanahifadhi bidhaa za vyakula na matumizi ya nyumbani katika jikoni. Kwa nini wasivihifadhii nje chini ya mti? Watasema kuwa vitaibwa au kuharibiwa na mvua, joto, na vumbi. Kubaliana na majibu yao. Waambie kwamba mbolea pia lazima **ishughulikiwe kwa hali ilio sahihi**.
2. Patia kila mshiriki kadi mbili za rangi. Eleza kwamba manjano inawakilisha *Fanya* na samawati inawakilisha *Usifanye*. Waambie kwamba utasoma kauli nyingi. Wataamua kama kila kauli ni **Fanya** au **Usifanye** kwa kuonyesha kadi zao.
3. Soma kauli zifuatazo moja kwa moja. Kila unaposoma kauli, wacha washiriki wainue kadi ya manjano (Fanya) au ya samawati (Usifanye). Kila mara uliza aliyeinua ya manjano na aliyeinua ya samawati kueleza ni kwa nini. Elezea kwa urahisi kwa nini ni *Fanya* au *Usifanye*.
4. Zifuatazo ndizo kauli za kusoma:
   - Unapokagua mbolea yako, tengeneza upya rekodi zako kabla ya kushughulikia mifuko yenye mashimo. **Usifanye**: Lazima uzishughulikie haraka ili kusimamisha kuendelea kumwagika, kuchafuliwa na kupoteza pesa.
   - Vitita katika sakafu kavu ya saruji. **Usifanye**: Saruji kavu huvuta unyevu kutoka chini na huenda ukaharibu mbolea. Mbolea ikishalowa, haitakuwa na matumizi tena.
   - Tumia vitita tofauti kwa aina tofauti za mbolea za mifuko. Wacha nafasi katikati ya kika aina. **Fanya**: Itasaidia kudhibiti mbolea alio nayo mkulima. Pia, mbolea zingine huenda zikageukiana kikemikali kama zitagusana.

- Fuata kanuni ya kwanza ndani – kwanza nje. **Fanya**: Itasaidia mbolea kutokaa sana ghalani na kukosa kuuzwa.
- Weka mbolea pamoja na petroli, mafuta na gesi. **Usifanye**: Mbolea zingine huenda zikashika moto kwa urahisi.
- Hakikisha mbolea ina vibandiko vilivyo sahihi vya maelezo. **Fanya**: Hii itasaidia kuzuia kuuzia mkulima mbolea isio sahihi na kuuza mbolea ghushi.
- Weka rekodi bora za matokeo ghalani. **Fanya**: Itazuia upotevu usiotakikana.
- Tumia mavazi ya kujikinga tu unapopokea mbolea. **Usifanye**: Wakati wowote unaposhughulikia mbolea tumia mavazi ya kujikinga.
- Agiza mbolea nyingi kushinda mahitaji yako kwa sababu wakulima wanaweza kutokea tu na kuinunu. **Usifanye**: epuka mbolea kuharibika mwishoni mwa msimu.
- Kubali tu mifuko ilioharibika kutoka kwa mchuuzi kama una uhakika unaweza kuzirekebisha. **Usifanye**: Ukikubali mifuko ilioharibika shida itakuwa yako.

# Malizia

**M**uhtasari: Peana muhtasari kwa kukariri Fanya na Usifanye vilivyo kwenye karatasi ya kufungua kurasa.

**M**aswali: Uliza kama yeyote ana swali au maoni.

**T**athmini: Uliza Fanya na Usifanye chache.

**H**atua fuatilizi: Katika kipindi hiki, tumejifunza kuhusu ushughulikiaji wa mbolea ulio sahihi. Katika moja ya vipindi vifuatavyo tutajadili uhifadhi wa pembejeo za ukulima katika maghala.

Sambaza **makaratasi ya taarifa ya maelezo** kwa washiriki wote.